## Je! Ninawezaje kusajili na kupata cheti cha kifo?

### Kifo kinachotokea katika vituo vya afya

Kifo kinapotokea katika kituo cha afya, msimamizi wa kituo cha afya hukodi kifo, anamjulisha afisa wa usajili, na kutoa taarifa ya kifo akithibitisha kutokea kwa kifo hicho katika kituo cha Afya.

### Kifo katika Jamii

Kifo kinapotokea katika jamii mkuu wa kaunti / karani wa Halmashauri ya mji  anaandika kifo hicho, anamjulisha ofisa wa usajili na kutoa rekodi ya taarifa ya kifo ikithibitisha kutokea kwa kifo hicho katika jamii.

## Mtu anahitaji nini kushughulikia cheti cha kifo?

1. Rikodi ya taarifa ya Kifo kutoka kwa kituo cha afya au kutoka kata / Divisheni.
2. Taarifa ya sababu ya kifo iliyotolewa na daktari aliyeshughulikia marehemu hospitalini au mwanapatholojia aliyefanya uchunguzi wa maiti.
3. Ambatisha nakala ya kitambulisho cha Taifa cha mwombaji na uwasilishe kitambulisho cha Taifa cha marehemu.
4. Risiti ya malipo ya shilingi 5000/= za Uganda kwa raia na dola 40 kwa wasio raia kutoka benki kwa jina la marehemu.
5. Hakuna malipo ya cheti kwa mkimbizi anayefariki nchini Uganda uthibitisho wa ukimbizi ukitolewa.

## USAJILI WA AMRI YA KUASILI NA KUTUNZA MTOTO

Kwa mujibu wa Sheria ya Watoto ni sharti kwamba msajili wa kizazi na vifo awe na daftari la Amri ya kuasili na Utunzaji ambamo mipango ya kuasili na utunzaji watoto itasajiliwa.

## Utaratibu wa kusajili Amri ya kuasili na kutunza mtoto.

1. Mwombaji anapata amri ya kuasili au kutunza mtoto kutoka kwa mahakama yenye mamlaka ya kutoa amri hiyo.
2. Wasilisha amri ya kuasili/kutunza mtoto kwa NIRA ili kupata cheti cha kuasili au uthibitisho wa usajili wa amri ya kutunza mtoto. Ambatisha nakala ya cheti cha kuzaliwa cha mtoto.
3. Ambatisha vitambulisho halali vya wazazi wanaoasili au mlezi wa kisheria kwa amri ya Utunzaji (nakala ya kitambulisho cha Taifa au Pasipoti)
4. Mwombaji atapewa cheti cha kuasili/ utaratibu bila malipo.


**NIRA (MAKAO MAKUU)**
Kiwanja cha Uhuru cha Taifa, Kololo Airstrip
S.L.P 26529, Kampala-Uganda
Simu (Mapokezi): +256 312119600

**Kwa Maulizo ya Wateja, wasiliana na:**
0800211700 (Kituo cha Simu)

**Kwa Maulizo juu ya Mahusiano ya Umma,**
Simu: +256 312119605

Nira_Ug   NIRA   nira.go.ug


NIRA
National Identification and Registration Authority
Uganda-My Country My Identity

# A QUICK GUIDE TO UNDERSTANDING THE CIVIL REGISTRATION SERVICES

## BIRTH/DEATH AND ADOPTION ORDERS REGISTRATION



# USAJILI WA KUZALIWA

Hii ndio kumbukumbu rasmi ya jina, jinsia, mahali pa kuzaliwa na kuzaliwa kwa mtu kama ilivyoamriwa na sheria. Katika usajili wa kuzaliwa, tunajibu ''nani'', ''wakati gani'', na ''kwa nini'' kuhusu mtu binafsi.

## Jinsi ya kupata cheti cha kuzaliwa

- Mtoto anapozaliwa katika kituo cha afya, msimamizi wa kituo hicho anamwaandika, na kutoa rikodi ya taarifa ya kuzaliwa.
- Mtoto anapozaliwa katika jamii, mkuu wa kaunti / karani wa Halmashauri ya mji anamwandika na kuweka kumbukumbu, anamjulisha Msajili, na kutoa rekodi ya taarifa ya kuzaliwa

Mama / baba / mdhamini hutembelea ofisi za NIRA za eneo hilo, na kuwasilisha vifuatavyo:

1. **Taarifa ya kuzaliwa kutoka kituo cha afya au kutoka kwa mkuu wa kaunti / karani wa Halmashauri ya mji.**
2. **Fomu 3 ya NIRA iliyojazwa na taarifa kamili ya kuzaliwa.**
3. **Vitambulisho vya Taifa / NIN za wazazi.**
4. **Risiti ya malipo ya shilingi 5000/= za Uganda kwa raia au dola 40 kwa wasio raia kutoka benki. Ni bure kwa wakimbizi.**

Mama / baba / mdhamini hupewa cheti cha kuzaliwa.

# KUPATA KITAMBULISHO KINGINE CHA KUZALIWA

Kupata nakala ya cheti chako cha kuzaliwa, ofisi yetu itahitaji kufanya utafutaji wa taarifa zilizopo. Utafutaji huo unafanywa baada ya malipo ya ada ya utaftaji ya dola 20 kwa wageni na Shilingi 1000 za Uganda kwa raia, na baada ya hapo unapewa matokeo. Tunahitaji nakala ya cheti cha awali au, taarifa ifuatayo kuwezesha utafutaji kwenye rekodi zetu:

1. Jina kamili
2. Tarehe ya kuzaliwa
3. Mahali pa kuzaliwa
4. Majina ya wazazi wa kibaolojia
5. Tarehe ya usajili / nambari ya usajili

Nakala ya cheti itashughulikiwa kwa ada ya dola 40 (wageni) na shilingi 5000 za Uganda (kitaifa). Zaidi ya hayo, tafadhali toa barua ya polisi kama uthibitisho wa kitambulisho kupotea na uambatishe nakala ya pasipoti / kitambulisho chako cha Taifa kama mtu anayeomba cheti.

**Taarifa iliyosemwa ikipatikana, tutaendelea kutoa nakala ya cheti cha kuzaliwa.**

## Jinsi ya kushughulikia cheti cha kuzaliwa ukiwa Ughaibuni

Ili kufanya malipo yaliyosemwa ukiwa ughaibuni, tembelea kwa urahisi wavuti wa Mamlaka ya Mapato ya Uganda kwenye ''**www.ura.go.ug**'' ili uweze kuona orodha ya Benki nje ya Uganda ambazo zinaweza kuweka pesa kwa akaunti yetu nchini Uganda.

**Ukifika kwenye wavuti,**

- **Bonyeza kwenye 'eService'.**
- **Chagua Usajili wa Malipo mkabala na malipo, na fomu itajitokeza.**
- **Kwenye fomu hiyo, chini ya Kichwa cha Ushuru, Chagua 'Nyingine NTR'.**
- **Tafadhali ruka aina nyingine zote na uende kwenye Sehemu ya Maelezo ya Benki.**
- **Chagua Njia ya Malipo unayopendelea.**

Orodha ya benki zilizoidhinishwa kulipia Kodi itaonekana. Chagua benki unayopendelea na ututumie jina lake kwa barua pepe ili tuweze kukutumia fomu za usajili wa malipo.

Vinginevyo, ikiwa una rafiki au jamaa anayeishi nchini Uganda na yuko tayari kukusaidia, tafadhali omba mtu huyo aje ofisini kwetu kwenye Uwanja wa Taifa wa Uhuru, Kololo Airstrip, achukue fomu za usajili wa malipo kati ya saa mbili asubuhi na saa kumi na moja jioni, Jumatatu hadi Ijumaa.

# USAJILI WA KIFO

## Usajili wa kifo ni nini?

Hii ni kumbukumbu rasmi ya jina, jinsia, mahali pa kifo, umri na sababu ya kifo cha mtu aliyekufa kama ilivyoamriwa na sheria. Katika usajili wa kifo tunajibu ''nani '', ''kwa nini'', ''wakati gani'', au ''vipi'' kuhusu marehemu.

## Nani ana jukumu la kutangaza kifo?

1. Ndugu au jamaa wa marehemu aliyekuwepo wakati wa kifo au;
2. Jamaa au ndugu wa marehemu anayeishi au aliyekuwa anaishi katika nyumba moja na marehemu;
3. Mtu anayepata au kushughulikia mwili wa marehemu au mtu anayeshughulikia mazishi ya marehemu kwa utaratibu huo